**HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI,MHESHIMIWA DK. ALI MOHAMED SHEIN,KATIKA UZINDUZI WA MRADI WA UWEKAJI WA LAINI YA PILI YA UMEME KUTOKA UBUNGO, DAR ES SALAAM HADI MTONI UNGUJA,UWANJA WA AMAAN**
**TAREHE 10 APRILI, 2013**

**Mheshimiwa Dk. Mohamed G. Bilali, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**
**Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar,**
**Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar,**
**Mheshimiwa Dk. Amani A. Karume, Rais Mstaafu wa Awamu ya Sita,**
**Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi,**
**Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar,**
**Waheshimiwa Mawaziri,**
**Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi,**
**Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**
**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi,**
**Mheshimiwa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Changamoto la Milenia,**
**Mheshimiwa Balozi wa Marekani Nchini Tanzania,**
**Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Nchi mbali mbali**
**Viongozi na Maofisa Mbali Mbali wa Serikali,**
**Wageni Waalikwa,**
**Mabibi na Mabwana,**

**Assalamu Alaykum**

**Awali ya yote, hatuna budi kumshukuru Mwenyenzi Mungu (SW) mwingi wa rehema na utukufu kwa kutupa uzima na kutuwezesha kukutana hapa katika siku hii muhimu sana ya kuzinduwa laini ya pili ya umeme kutoka Ubungo Dar-es-salaam hadi Mtoni, Unguja. Napenda kutumia fursa hii kukukaribisheni wageni wetu na waalikwa wote. Aidha, natoa shukurani za dhati kwa maandalizi mazuri ya sherehe hizi na vile vile nakupongezeni ndugu wananchi kwa mahudhurio yenu mazuri katika hafla hii muhimu ya kimaendeleo hapa Zanzibar. Nakushukuruni sana!**

**Ndugu Wananchi,**

**Mtakumbuka kuwa mnamo mwezi wa Oktoba mwaka 2012, baadhi yenu tulikutana Fumba kwa ajili ya kuzindua ulazaji wa waya wa pili wa umeme kutoka Ras Fumba hadi Ras Kilomoni Tanzania Bara. Wakati nazindua ulazaji huo wa waya wa pili, nilisema kuwa mwelekeo wa kuwa na umeme wa uhakika umeonesha dalili nzuri na tatizo la mgao wa umeme litamalizika hivi karibuni. Ikumbukwe kuwa nilisema hayo mwaka jana.**

**Mwaka huu, 2013 na hasa leo tuna kila sababu ya kufurahia na kujipongeza kwa mafanikio haya ya kufanikisha mradi huu kwa ufanisi mkubwa.**

**Ndugu Wananchi,**

**Sherehe zetu za leo ni hitimisho la mchakato mrefu ulioanza katika Awamu ya Tatu katika uongozi wa Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin Mkapa na Awamu ya Sita ya Rais Mstaafu Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume na tangu mwezi wa Februari mwaka 2008 baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. Jakaya Mrisho Kikwete na aliyekuwa Rais wa Marekani, Mhe. George W. Bush walipotia saini mkataba wa Millenium Challenge Compact wenye thamani ya dola milioni 698.1 kwa madhumuni kupunguza umaskini kupitia uwekezaji katika sekta ya usafirishaji, nishati ya umeme na uwekezaji katika sekta ya maji. Kwa maana hiyo, mradi huu ni kielelezo cha kutosha cha kuwa tumedhamiria kwa dhati kuupiga vita umaskini hapa Zanzibar na Tanzania nzima kwa jumla.**

**Kukamilika kwa mradi huu vile vile ni kielelezo cha urafiki baina ya Marekani na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hasa Zanzibar. Urafiki wa watu wa Marekani na Zanzibar haukukomea kwenye nishati ya umeme peke yake bali Shirika la Changamoto za Milenia kadhalika linasaidia ujenzi wa kilometa 35 za barabara huko Pemba katika kiwango cha lami. Aidha, Serikali ya Marekani inashirikiana na Zanzibar katika sekta ya afya katika kupambana na malaria, kifua**

**kikuu na ukimwi. Kama kawaida yetu ya kufanya mambo kwa ufanisi, tumeweza kutokomeza maradhi ya malaria kwa kiwango kikubwa cha chini ya asilimia moja. Nchi yetu hivi sasa inatumika kama kigezo cha ufanisi katika kupambana na malaria. Hayo ni mafanikio makubwa na tunapaswa kuyaendeleza.**

**Napenda kutoa shukurani zangu za dhati na za wananchi wa Zanzibar kwa Serikali na watu wa Marekani kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa kupitia Balozi wa Marekani nchini Bwana Alfonso Lenhardt ambae amekuwa nasi mara kwa mara katika utekelezaji wa miradi mbali mbali inayosimamiwa kwa pamoja kati yetu na mashirika ya misaada ya Marekani ikiwa ni pamoja na USAID. Hivi karibuni Serikali ya Marekani kwa kushirikiana na DANIDA walitusaidia katika ujenzi wa ghala kuu la dawa tuliyoifungua mwezi wa Januari mwaka huu kule Maruhubi.**

**Aidha, tumekuwa pamoja na Balozi Lenhardt katika uzinduzi wa mradi wa elimu ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa skuli za msingi ujulikanao kama T21 uliofanyika mwezi Febuari mwaka 2012 katika Skuli ya Mwanakwerekwe C. Kadhalika, kuhusiana na mradi huu wa umeme tunaouzindua leo, tumekuwa tukishirikiana na Balozi Lenhardt hatua kwa hatua hadi hatua hii ya leo ya uzinduzi. Balozi Alfonso kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar nasema ahsante sana.**

**Ndugu Wananchi,**

**Sote ni mashahidi wa kilichotokea katika kipindi cha mwezi wa Mei na Juni mwaka 2008 wakati ilipotokea hitilafu ya umeme katika Kituo cha Fumba na kusababisha kukosa umeme kwa kipindi cha takriban miezi mitatu. Hali kama hiyo ilitokea tena mnamo Disemba ya mwaka 2009. Matukio hayo mawili yalileta madhara makubwa katika masuala ya kijamii na kiuchumi. Athari nyingi zilijitokeza katika utoaji wa huduma za afya, upatikanaji wa huduma ya maji, shughuli za biashara, utalii, uzalishaji viwandani, maofisini na hata kukosa umeme kwa matumizi yetu ya majumbani.**

**Nyote ni mashahidi kuwa Serikali ilijitahidi kikamilifu kuhakikisha kuwa umeme unarudi katika hali ya kawaida kwa haraka iwezekanavyo. Ingawa juhudi hizo zilizaa matunda lakini ukweli ni kwamba waya wa zamani ulikuwa mkuu kuu mno. Waya huu ulikuwa na uwezo wa kuchukua megawati 45 wakati mahitaji yetu ya umeme yalikwishafikia megawati 50. Tofauti hii ilisababisha kuwepo kwa mgao wa dharura wa umeme jambo ambalo lilileta usumbufu ingawaje lilifanywa pasipo budi.**

**Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi wote kwa kuelewa na ustahamilivu wenu mliouonesha katika kipindi chote cha kuwepo kwa mgao wa dharura wa umeme. Lakini wahenga walisema "Baada ya dhiki faraja". Leo faraja imeshafikiwa kwa kuzindua laini ya pili ya umeme wa megawati 100. Kwa hakika "Mvumilivu hula mbivu". Leo sote tunastahiki kula mbivu hiyo. Hongereni Sana!**

**Ndugu Wananchi**

**Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, katika taarifa yake ya kitaalamu, alieleza kuwa megawati 100 ni mara mbili ya mahitaji yetu. Kwa maana hiyo, waya huu wa pili utalipa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) uwezo mara mbili wa kuongeza wateja wa Shirika. Nawasihi sana watendaji wa ZECO watumie vyema ongezeko hili la uwezo wao na kuimarisha huduma zao kwa wateja na kuongeza mapato. Hii itakuwa ndio namna bora ya kuonesha tofauti iliyokuwepo kabla na baada ya Shirika la ZECO kupata uwezo zaidi . Ongezeko la idadi ya watumiaji wa umeme la asilimia saba bado halitoshi. Nashauri ule utaratibu wa kuwapatia mkopo wa kuungiwa umeme wananchi wa kipato cha chini uzidi kutiliwa mkazo hasa kwa wananchi wanaoishi vijijini ili nao waweze kunufaika na huduma hizi muhimu.**

**Kadhalika, napenda kuliagiza Shirika la Umeme kuendelea na kampeni zake za kuwadhibiti wale wote wanaounga umeme bila ya kufuata taratibu na kuwachukulia hatua za kisheria. Aidha, ni muhimu kuongeza kasi na juhudi za kukusanya madeni kutoka kwa wateja hasa wale wanaoghafilika katika kulipa**

**madeni yao. Si vyema kutumia huduma za umeme lakini ukasahau wakati wa kulipa. Kupata huduma ya matumizi ya umeme ni haki ya wateja lakini nao watimize wajibu wao wa kulipia gharama za umeme. Tuzingatie usemi maarufu kwamba: "Haki na Wajibu ni Watoto Pacha". Kulipa madeni kwa wakati kutaliwezesha Shirika la Umeme (ZECO) kuimarisha huduma zake ipasavyo.**

**Itakumbukwa kuwa waya huu wa umeme vile vile umetoa fursa kwa nchi yetu kuunganishwa kimawasiliano na mkongo wa mawasiliano wa kimataifa uliopo Tanzania Bara. Nasi kwa upande wetu tumeshajitayarisha kuziunganisha taasisi zote za Serikali kimtandao chini ya Mradi wa "e-Government" ambao tuliuzindua rasmi wakati wa Sherehe za Mapinduzi za Januari, 2013.**

**Ndugu Wananchi,**

**Kukamilika kwa mradi huu na ule wa kukiunganisha Kisiwa cha Pemba na Gridi ya Taifa kunaifanya Zanzibar nzima kuwa na umeme wa uhakika. Kwa hivyo, mradi huu unatoa mchango mkubwa katika kutimiza malengo yetu ya maendeleo kama yalivyoelezwa katika Dira ya Maendeleo ya 2020, Mpango wa Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA), Mpango wa Kimataifa wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia na vile vile kutekeleza ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010.**

**Aidha, matarajio ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuwa wawekezaji wengi zaidi wa ndani na nje wataweza kuwekeza na kupanua sekta za uwekezaji nchini mwetu kwani changamoto kubwa iliyokuwa inatukabili kwa wawekezaji hawa ni ukosefu wa umeme wa uhakika. Nawasihi wananchi watumie fursa hii ya umeme wa uhakika kuongeza uzalishaji zaidi na vile vile kuanzisha shughuli mbali mbali za kujiajiri wenyewe na kuzalisha bidhaa kwa matumizi yetu na kuuza nje ya nchi. Aidha, wale ambao bado hawajaunganishiwa umeme, nao wajiandae na waitumie fursa hii kupata umeme. Kwa hakika umeme ni kwa ajili ya maendeleo. Hivyo, ni vyema sote tukafaidika na fursa hii kwa kuimarisha maendeleo yetu kuanzia ngazi ya Kaya, Shehia, Wilaya, Mikoa hadi nchi nzima.**

**Ndugu Wananchi,**

**Imeelezwa kwamba kuwa mradi huu hadi kukamilika kwake umegharimu jumla dola za Marekani milioni 64.4 na Zanzibar imechangia karibu dola za Marekani milioni moja na nusu. Hizi sio fedha kidogo na ni fedha za walipa kodi wa Marekani na wa hapa Zanzibar. Kwa hivyo, napenda kusisitiza kuwa wananchi wote tuna jukumu kubwa la kulinda miundo mbinu ya usambazaji wa umeme hapa Zanzibar bila ya kujali kama ni mipya au ya zamani.**

**Nasema hivyo kwa sababu, hivi sasa kumejitokeza tabia mbaya ya uharibifu wa miundo mbinu ya umeme na kuathiri usambazaji wa umeme. Kuna baadhi ya watu wanaiba nyaya za umeme na wengine huchimba mchanga chini ya nguzo za umeme. Jambo hili siyo tu linaathiri mazingira bali linaweza kusababisha maafa makubwa ikiwa nguzo hizi za umeme mkubwa zitaanguka. Mungu atuepushe na kadhia hiyo.**

**Nawasihi sana wananchi wenye tabia hiyo waache kabisa. Nazikumbusha mamlaka zinazohusika kama vile Idara ya Mazingira na Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Mkoa wa mjini Magharibi kuandaa kampeni maalum ya kuwafuatilia wachimbaji udongo na mchanga bila ruhusa ya Serikali na kuwachukulia hatua za kisheria. Aidha, nawasihi wananchi mnaokaa katika maeneo ambayo nguzo za umeme zipo na uchimbaji usioruhusiwa wa mchanga unafanyika muwe walinzi shirikishi na mtoe taarifa kwa vyombo vinavyohusika.**

**Ndugu Wananchi,**

**Kwa hakika leo ni leo na wale waliyosema hayawi sasa yamekuwa. Leo sio siku ya hotuba ndefu, bali ni siku ya kubainisha zaidi furaha zetu. Hata hivyo, haitokuwa jambo jema kama sitachukua fursa hii kutoa shukurani za dhati kwa Serikali ya Marekani na Shirika la Changamoto la Milenia na MCA–T kwa kushirikiana nasi kwa karibu hadi kufikia hatua hii ya leo. Ni matumaini yetu kuwa Zanzibar itaingia katika awamu ya pili ya "Millenium Challenge Compact" jambo ambalo litatupa faraja zaidi.**

**Napenda kutoa shukurani kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Wizara ya Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati, Shirika la Umeme Zanzibar – ZECO, TANESCO, viongozi wa Serikali za mitaa pamoja na wananchi wa maeneo ambayo mradi huu umepita. Maeneo hayo ni pamoja na Fumba, Dimani, Kombeni, Maungani, Kijito Upele, Mwanakwerekwe, Welezo na Karakana. Vile vile, natoa shukurani kwa masheha na viongozi wengine kwa juhudi zao na mashirikiano makubwa waliyotoa wakati wa utekelezaji wa mradi huu. Shukrani zangu za dhati nataka nizitoe kwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Sita wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Jakaya Kikwete kwa jitihada zao kuifanikisha Miradi ya MCC. Kadhalika, shukrani zangu nazitoa kwa Rais wa Marekani Mheshimiwa Barak Obama kwa kutuunga mkono kwa mipango yetu ya maendeleo. Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba inathamini sana juhudi hizo ambapo leo tunaadhimisha kukamilika kwa utekelezaji wa mradi wetu huu kwa mafanikio makubwa.**

**Namalizia hotuba yangu kwa kukushukuruni tena wananchi nyote mliohudhuria sherehe hii wakiwemo viongozi na watendaji mbali mbali wa Serikali na vyama vya siasa. Vile vile, napenda nitoe shukurani kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Changamoto za Milenia (MCC) Mr. Daniel Wolde Yohannes na wataalamu wetu wazalendo waliofanyakazi katika mradi huu na wawakilishi wa Taasisi za kiraia waliojumuika nasi katika sherehe hizi. Kuwepo kwenu nyote katika hafla hii kumezidi kuifanya shughuli yetu hii muhimu na ya kihistoria kuwa ya kupendeza zaidi. Shukurani maalum kwa vikundi vyetu vya utamaduni, wasanii wetu wote na hasa IT, ahsanteni kwa CD yenu.**

**Tumuombe Mwenyezi Mungu Mtukufu atuzidishie amani, umoja na mshikamano nchini. Atupe uwezo na nguvu za kutekeleza vyema mipango yetu ya maendeleo kwa ufanisi mkubwa. Mola wetu atujaalie sote turudi nyumbani salama na atukutanishe tena mara nyengine.**

**MUNGU IBARIKI ZANZIBAR,**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA,**

**MAPINDUZI DAIMA.**

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.**